

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALAMSHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA**



Kumb.Na.LG.L.10/11/83

28/03/2018

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kwa mujibu wa kibali cha ajira Kumb. Na.CFC 26/205/01“FF”/91 cha tarehe 22.08.2017 kama kilivyoongezewa muda kwa kibali cha Kumb. Na. Na.CFC 26/205/01 “GG” /95 12.03.2018 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea

**1. MTENDAJI WA KIJIKI III – NAFASI HAMSINI NA TATU (53)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Mwombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashahada /Cheti “NTA level 5” katika fani zifuatazo;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmshauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.

- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika kijiji.
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za kijiji,

### **MSHAHARA**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina mshahara ni TGS B Sawa na Tsh. 390,000/=


### **MASHARTI YA JUMLA**

- i. Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutuma kwenye anuani iliyotajwa hapo chini.
- iii. Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iv. Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma na ana sifa za kuingilia katika kada tofauti na aliyonayo apitishie barua yake ya maombi kwa Muajiri wake kuthibitisha kuridhia.
- v. Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (a detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- vi. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:
  - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV au VI.
  - Cheti cha mafunzo (professional).
  - Cheti cha kuzaliwa.
  - Picha Moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- vii. "Testimonials", " Provisional results", "Statement of results ", hati matokeo za kidato cha IV na VI (form IV AND form VI results slips) **HAVITAKUBALIWA.**

- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **10/04/2018 saa 9:30** alasiri.
- x. Watakaoitwa kwenye usaili majina yao yatawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ([www.nachingweadc.go.tz](http://www.nachingweadc.go.tz))
- xi. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kishwahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo.

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI WA WILAYA,  
S.LP 291,  
**NACHINGWEA.**

Limetolewa na:

  
Kiwale A.T

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**NACHINGWEA**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI WA WILAYA  
NACHINGWEA

**Nakala:**

- Mbao za Matangazo
- Tovuti ya Halmashauri ([www.nachingweadc.go.tz](http://www.nachingweadc.go.tz))